## *ISAAA Yaadhimisha Maisha ya Mlezi na Mwanzilishi, na Mshindi wa Tuzo la Amani la Nobel*


Baba wa Mapinduzi ya Kijani

•••

Mtetezi wa wakulima Maskini na wenye pato dogo katika nchi zinazoendelea

•••

Mwanzilishi wa *Tuzo la Chakula Duniani*



# *Norman Borlaug*

***1914 - 2009***

ISAAA
INTERNATIONAL SERVICE FOR THE ACQUISITION OF AGRI-BIOTECH APPLICATIONS










## *Urithi na Mchango wa Dkt Norman Borlaug*

Dkt. Norman Borlaug mtaalamu kielelezo wa ustawishaji wa kilimo kwa manufaa ya maskini aliaga dunia Septemba 12, 2009 akiwa na umri wa miaka 95. Alizaliwa Cresco, Iowa kule Marekani. Kujitolea kwake kibinafsi na kitaaluma kupambana na njaa na umaskini, akianzisha kazi kuhusu aina bora za ngano zilizoweza kuhimili magonjwa mbalimbali na zinazoweza kuzalisha mazao bora kwa kutumia sayansi ya bayoteknolojia

## *Tuzo la Amani la Nobel*

Katika mwaka wa 1970, *Tuzo la Amani la Nobel* lilituzwa Dkt. Norman Borlaug na kamati husika ikahitimisha hivi: 'Zaidi ya watu wa wakati wake, alisaidia kuwapa lishe wenye njaa duniani. Tumefanya uteuzi huu kwa tumaini kuwa utoaji wa lishe au riziki utaleta amani duniani. Amechangia kuvumbua hali mpya ya chakula duniani ambapo ameweza kubadilisha hali ya kutamauka kuwa ya matumaini katika hali ya vuta nikuvute ya mashindano kati ya mfumko wa idadi ya watu na uzalishaji wetu wa chakula.

## *Utetezi wa Nguvu wa Norman Borlaug wa Bayoteki/Ugeuzi wa Jeni na Uboreshaji Mazao na Mchango Wake kwa Usalama wa Chakula na Uangamizi wa Njaa na Umaskini Ulimwenguni*

Akituzwa *Tuzo la Amani la Nobel* kwa kuokoa watu bilioni moja kutokana na baa la njaa, Norman Borlaug kwa hekima aliukumbusha ulimwengu kuwa juhudi zake zilileta suluhisho "la muda tu" na kilichohitajika ni uwekezaji katika uimarishaji wa teknolojia ya kilimo, jambo ambalo lilikuwa ni la "lazima" ili kushibisha dunia ya kesho. "Norm", kama vile alivyopenda kujulikana na Jeshi lake la marafiki kote dunia, alikuwa mtetezi wa dhati wa bayoteki /ugeuzi jeni na uboreshaji mazao (GM), ambayo alionelea kuwa moja ya nyenzo muhimu za teknolojia kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa chakula siku zijazo.

Aliangazia kuwa ***"kwa kipindi cha mwongo mmoja uliyopita, tumeshuhudia uimarikaji wa zao la bayoteknolojia. Teknolojia hii inasaidia wakulima ulimwenguni kote kuzalisha mazao ya juu, wakati wakipunguza matumizi ya dawa za wadudu pia kuzuia mmomonyoko wa udongo. Faida na usalama wa bayoteknolojia umethibitika muongo uliopita katika nchi zilizo na zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani. Tunachohitaji ni ujasiri wa viongozi wa nchi ambazo wakulima bado hawana chaguo bali kutumia mbinu zilizopitwa na wakati na zenye ufanisi wa chini. Mapinduzi ya Kijani na sasa upanzi zao bayoteknolojia vinasaidia kukidhi ongezeko la mahitaji kwa uzalishaji wa chakula, wakati zikihifadhi mazingira yetu kwa vizazi vijavyo.***

## *Tuzo la Chakula Duniani*

Mwaka 1986 Norman Borlaug alianzisha *Tuzo la Chakula Duniani*, ambalo awali iliungwa mkono na kampuni ya *General Foods* kwa miaka mitatu, na kisha namunufaiki wake wa sasa, Juan Ruan, mwanabiashara kutoka Des Moines, Iowa, ambaye aliyejaliwa ukarimu wa kutunza

kufadhili *Tuzo la Chakula Duniani* milele. Sherehe za *Tuzo la Chakula Duniani* hufanyika Oktoba kila mwaka, ziki shirikiana na Kongamano la Borlaug na tukio la *Tuzo la Chakula Duniani*, Taasisi ya vijana, kwa ajili ya kusaidia kuendeleza viongozi wa baadaye. Tuzo hili la heshima la Chakula Duniani hutambuliwa "Tuzo la Nobel la Chakula ". Limekabidhiwa wapokeaji wa kuheshimika kutoka duniani kote ambao wamechangia mchango wa kipekee kwenye utoaji chakula duniani.

**Dkt M.S. Swaminathan, mwenzake Borlaug katika vuguvugu la Mapinduzi ya Kijani India, ndiye mpokeaji wa kwanza wa *Tuzo la Chakula Duniani* mnamo mwaka wa 1987. Dr Swaminathan pia ni mwanzilishi wa ISAAA.**


## *Uanzishaji wa kituo cha ISAAA cha Maarifa Kiutandawazi (KC) cha Mazao bayoteki*

### *Maarifa • Teknolojia*
### *Kupunguza Umaskini*

Mwaka wa 2000, Dkt Borlaug akiandamana na mwanzilishi aidha mwenyekiti wa ISAAA Dkt Clive James na mratibu wa dunia Randy Hautea, na maafisa wa serikali ya Ufilipino walikutana na Akademia ya taifa ya sayansi na teknolojia ili kubadilishana nao maoni yake na changamoto kuhusu tatizo sugu la utoshelevu wa chakula na inavyohusika sayansi na teknolojia katika kukabililana na hali hiyo. Katika hafla hiyo, alitunukiwa uanachama wa heshima wa NAST. Katika ziara hii ya Ufilipino, Norman Borlaug aliunga mkono juhudi za ISAAA za kusambaza mbinu mpya za kitaaluma kwa kuanzisha kituo cha ‘Global Knowledge’ kushughulikia bayoteknolojia ya mimea.

**Kama bendera ya meli, Ripoti ya kituo cha Maarifa cha ISAAA ni chapisho la mwaka kuhusu kiwango cha mazao ya Kibayoteki/yaliyoboreshwa kwa ugeuzi jeni lililoandikwa na Clive James - linashangaza, matokeo makuu ya taarifa ya 2007 ilifikia watu bilioni 1.1 (asilimia 16% ya idadi ya watu ulimwenguni) kwenye nchi zaidi ya 70, na kwa lugha zaidi ya 40.**
**Kazi nyingine ya manufaa iliyotokana na kituo hiki cha maarifa cha ISAAA ni uchapishaji wa barua pepe kuhusu bayotekinolojia ya mimea ambayo katika kila wiki, husambazwa kwa wasomaji 650,000 katika nchi 200, usambazaji ambao umekua kufikia wasomaji takribani 5,000 kila mwezi.**

## *Sifa Maalum kwa Norm Borlaug na Clive James, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa ISAAA*



5

Norm daima atakumbukwa kwa kuwa mwanachama wa aina yake katika familia ya ISAAA kwa sababu ya hulka yake ya kipekee, uwajibikaji na mchango wake katika kuboresha maisha ya mamilioni ya watu maskini ulimwenguni.



6

Hizi ni shukrani maalum katika shairi huru kutoka ISAAA, ilioandikwa na Dkt Clive James (Mwanzilishi na Mwenyekiti wa ISAAA na aidha alikuwa naibu wa mkurugenzi mkuu wa CIMMYT Meksiko). Kama kumbukumbu ya Norman Borlaug aliyekuwa mshauri wake na rafiki wa kipekee kwake kwa miaka 30 - shairi hili limechukuliwa kutoka kwa shairi lililo tungwa na Huexotzin, mwana wa mfalme wa Texcoco, Meksiko, Circa. Mnamo mwaka wa 1484 akiomboleza kifo cha babu yake, mfalme Nezahualcoyotl mashuhuri ambaye kama mjukuu wake Huexotzin alikuwa amesomea elimu mimea na pia mshairi. Kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo Norman Borlaug ya Meksiko, huenda angeona fahari kutambuliwa kama mwana wa kifalme wa Texcoco na bonde la Yagui - Sonara,sehemu alizotumikia kwa zaidi ya miaka 50. Mara kwa mara alikuwa akisema haya kuhusu bonde la Yagui

***“Hapa ndipo kwa kweli na jihisi nipo nyumbani na ndipo nilipo na amani.”***

**" Mkate wa Mbinguni* – Tulishe hadi tusaze"**

*Waniambia lazima niangamie*
*Kama mamilioni niliosaidia kulisha*
*Jambo linalokumbukwa la jina langu*
*Jambo linalokumbukwa la umaarufu wangu*
*Lakini ngano niliyokuza Meksiko ingali changa*
*Na chembe za ukuzi za Yagui zitaendeleza wimbo wa kiutu*

*" Mkate wa Mbinguni" ndio wimbo wa Kiingereza uliosifika huimbwao katika sherehe za kitaifa kama vile mazishi ya Binti Mfalme Diana na huteka lengo kuu aliloshikilia maishani – kumaliza tatizo la njaa.

*Picha kwa niamba ya*
*1. Kituo cha Kuboresha Mahindi na Ngano cha Kimataifa (CIMMYT), Meksiko*
*2. Baraza la kindi la Utafiti wa Kilimo (ICAR), India*
*3. Kituo cha Kuboresha Mahindi na Ngano cha Kimataifa (CIMMYT), Meksiko*
*4. Baraza la kindi la Utafiti wa Kilimo (ICAR), India*
*5. Kituo cha Tuzo ya Amani cha Msingi wa Tuzo, Norway*
*6. Huduma za Kimataifa za Upataji na Utumizi wa Kilimo cha Kibayoteki (ISAAA)*

ISAAA
INTERNATIONAL SERVICE FOR THE ACQUISITION OF AGRI-BIOTECH APPLICATIONS

Kwa maelezo zaidi: ISAAA AfriCenter, P.O. Box 70, ILRI Campus, Old Naivasha Rd.
Uthiru, Nairobi 00605, Phone: +254-20-4223618, Fax: +254-20-4223634, Email: africenter@isaaa.org